Toleo 55 - Dhul Hijjah 1442 AH / Agosti 2021 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Pongezi Kutoka kwa Hizb ut Tahrir kwa Idd Al-Adha Al-Mubarak

**MAKALA**
Tume ya Uajiri wa Walimu (TSC)

**TOLEO JIPYA**
Ukatili wa Kijinsia ni Natija ya Sera ya Usawa wa Kijinsia ya Kimagharibi

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Uzinduzi Rasmi wa Kampeni ya Kiuchumi ya Hizb ut-Tahrir Kenya



Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴾

Hizb ut Tahrir

KUMB: 15/1442 | Alhamisi, 27 Dhu al-Qi'dah 1442 H | 08/07/2021 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Uzinduzi Rasmi wa Kampeni ya Kiuchumi ya Hizb ut-Tahrir / Kenya Chini ya Kauli Mbiu: Msoto wa Kiuchumi: Uislamu Ndio Jibu.

Harakati ya Hizb ut-Tahrir Kenya imezindua rasmi kampeni ya kiuchumi itakayodumu kwa mwezi mmoja. Kampeni hii itaanza tarehe mosi ya mwezi mtukufu wa DhulHijja 1442 Hijria sawasawa na tarehe 11 Julai 2021 na kutamatika Agosti 11.

Kampeni hii inalenga kuangazia uhalisia wa mfumo wa Kiuchumi wa Kibepari na jinsi ulivyosababishia umma majanga ya kiuchumi. Aidha, inalenga kuweka wazi uhalisia wa mfumo wa Kiuchumi wa Kiislamu na athari yake katika kipindi cha karne 13 pindi Uislamu ulipokuwa na utawala wake wa Khilafah pia na vipi pindi itakaposimama hivi karibuni kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu SWT itaweza kutatua matatizo ya kiuchumi na mengineyo.

Kwenye kampeni hii, Hizb ut-Tahrir / Kenya itaandaa msururu wa amali ikiwemo mihadhara mbalimbali katika maeneo mbalimbali, mazungumzo ya mitaani, semina na wasomi na mufakirina miongoni mwa amali nyengine.

Mwisho, tunatoa mwito kwa jamii kwa jumla na hasa Umma wa Kiislamu kushiriki nasi katika kampeni hii tukufu ambayo ndani yake hatutarajii lolote ila malipo kwa Mwenyezi Mungu SWT. Twamuomba Mwenyezi Mungu (swt) afanikishe kampeni hii na ifanye kuwa ni yenye kuleta kheri kwa Umma wote wa Kiislamu.

**Fuatilia Kampeni hii kwa Hashtag:**

Kiswahili: #MsotowaKiuchumi_Uislamundio_Jibu

Kiingereza: #EconomicHardships_IslamIsTheSolution

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**

Afisi kuu ya
Habari ya
Hizb ut Tahrir

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 45/1442 | Jumanne, 10 Dhu al-Hijjah 1442 H | 20/07/2021 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Pongezi Kutoka kwa Hizb ut Tahrir kwa Idd Al-Adha Al-Mubarak

**Allahu Akbar Allahu Akbar Allahu Akbar La Ilaha Ila Allah Allahu Akbar Allahu Akbar Wa Lilahi Alhamd**

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu, na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote, Anayeleta bishara njema ya ushindi na tamkini, na Muonyaji kwa Aya Tukufu. Rehma na amani zimshukie yule aliyeturithisha sheria ambayo kwayo nyoyo ziling'aa, akili kuangazwa, na hali kutengea, na kutuwekea Khilafah ambayo kwayo nchi zilipanuka, maisha yalinawirika, na jamii ziliunganishwa kama ndugu… Bwana wetu, Bwana wa viumbe vyote Muhammad na jamaa zake na maswahaba zake.

Furaha ya wale wanaopeana mikono baada ya swala ya Idd, furaha ya watoto katika nyumba za Waislamu, furaha ya waja watiifu na matunda yao ya siku kumi za Dhu al-Hijjah, utolewaji sadaka kwa Al-Aziz Al-Jabbar, na furaha ya kumaliza ibada kwa wale walioweza kufikia njia ya Nyumba Takatifu.

Kongoni kwa Idd Al-Adha… Kongoni kwa furaha ambayo huleta utulivu wa nyoyo… Kongoni kwa bishara ya faraja iliyo karibia...

Katika mnasaba huu uliobarikiwa, ninafuraha kutoa pongezi maalum kutoka kwa wanachama wa Hizb ut Tahrir, kwa Ummah bora ambayo ilioletwa kwa watu, Ummah wa Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, tukimuomba Mwenyezi Mungu aifanye furaha ya Idd hii iwe ni bishara za karibu na ushindi dhahiri.

Pia natoa pongezi maalum kwa niaba yangu na kwa niaba ya mkuu wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na wafanyikazi wake wote, kwa Amiri wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni mkubwa, Ata bin Khalil Abu Al-Rashtah, tukimuomba Mwenyezi Mungu amwafikie katika kuiongoza dawah na kuomba Nusra (msaada wa kijeshi) kwa ajili ya kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume.

**Enyi Waislamu:**

Mwenyezi Mungu amewachagua watu ndani ya mataifa ambao wanaweza kutambua uhalisia wao, wakiwasiliana na hisia zao, na kuelezea hali yao. Wakati wale ambao Mwenyezi Mungu amewajaalia na uwezo huu wanapoongoza njia katika kuwahutubia na kuwashauri watu wao, huziteka nyoyo na akili za watu, na kuwa ndio wanaounda rai jumla kwa watu wao. Kwenye Iddi hii, tutawahutubia wao haswa, kuwakumbusha umuhimu wa dori yao, na kwa Ummah kujua haki yake kwao.

**Kwa Waundaji wote wa Rai Jumla katika Umma wa Kiislamu:**

Mnayo majukwaa, wavuti, kalamu, kurasa, vituo, magazeti, vipindi na majukwaa ya vyombo vya habari, majukwaa ya Dawah na yasiyo ya Dawah, na aina zote za watengenezaji maalumati kwenye vyombo vya habari, wale miongoni mwenu ambao wamekuuzwa katika mambo ya Uislamu, na wale miongoni mwenu ambao wamekuuzwa juu ya maswala ya maisha na maswala ya watu na ambao hufanya mambo mazito ya kimaisha na hata burudani: Tunawahutubia nyinyi nyote katika Idd hii katika wadhifa wenu kama wale waliokubali jukumu la kushauri, kutoa maoni na kuziongoza hisia za watu Umma wa Kiislamu. Mtume (saw) asema:

«أَيُّمَا دَاعٍ دَعَا إِلَى شَيْءٍ كَانَ مَوْقُوفاً مَعَهُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ، لَا يُغَادِرُهُ وَلَا يُفَارِقُهُ، وَإِنْ دَعَا رَجُلٌ رَجُلًا. ثُمَّ قَرَأَ: ﴿وَقِفُوهُمْ إِنَّهُمْ مَسْئُولُونَ﴾»

“Pindi mtu anapolingania kitu, kitakuwa pamoja naye hadi Siku ya Kiyama, hakitamuacha wala kutengana naye, hata kama mtu atamlingania mtu mwengine. Kisha akasoma: “Na wasimamisheni. Hakika hao watasailiwa.”[As-Saffat: 24].

***Endelea... UK 4***

 Email: info@uqab.or.ke

Tunauhakika na uhalisia wa mambo matatu kwamba utambuzi jumla na rai jumla ya watu wa Umma wa Kiislamu zimeyafikia:

**Uhalisia wa kwanza:** ni kwamba Umma umetambua barabara kwa Uislamu ndio njia anayoiridhia Mwenyezi Mungu (swt) kwa maisha ya wanadamu.

**Uhalisia wa pili:** ni kwamba Umma, baada ya karne moja ya mapambano ya gharama kubwa, umetambua barabara kuwa izza yake ufanisi wake hauna budi zimefungamana na uwepo wa Khilafah ya Kiislamu.

**Uhalisia wa tatu:** ni kwamba Umma wa Kiislamu una hamu ya kurudi kwa utawala muongofu wa Uislamu kama ilivyokuwa wakati wa Maswahaba watukufu. Bali, uko tayari kupambana na kutoa roho zake na roho za watoto wake kwa ajili ya jambo hili endapo utadiriki na una yakini kuhusu njia ya kupata hilo.

Tunahakika na uhalisia huu kuhusu rai jumla ya sasa ya Umma wa Kiislamu, lakini uhalisia huu hautoshi kudhibiti maendeleo ya Ummah kwenye njia ya wokovu. Badala yake, inahitaji mtu kuusaidia kujua ufafanuzi wa mfumo wa Kiislamu wakati unapokabiliwa na njama na changamoto. **Hapa inakuja dori ya waundaji wa rai jumla** kutoka kwa wana wa Umma wa Kiislamu. Kuupatia Umma maelezo ya fikra ya Kiislamu. Hapa lazima tutaje mifano inayoonyesha umuhimu na uzito wa jukumu hili.

Mfano wa hili ni wakati muundaji rai - anayependa na kutamani umoja wa Umma wa Kiislamu - anapopuuza wakati uzalendo unapowasilishwa kama fikra ya kisiasa katika nyenzo anazowasilisha kwa hadhira yake, au kwamba anaunga mkono wajibu wa kuheshimu ubwana wa mataifa katika nchi za Kiislamu, kama sheria za kutoa na kunyima uraia na visa za usafiri, kwa Waislamu kutoka nchi zengine na anasahau kuwa fikra ya utaifa na sheria zinazotokana na ubwana wa kitaifa sio chochote ila ni fikra hatari za kisiasa, kusudi lao ni kuigonga fikra ya umoja wa Umma wa Kiislamu. Badala yake, alipaswa kutaja uharamu wa uzalendo na kuonya umma wake juu ya hatari yake. Badala yake, hakupaswa kulegea kujielimisha kwa kina kinachostahili ili kuwasilisha kwa umma wake ufahamu wa utiifu wa kibinadamu kwa watu wa nchi yake na maslahi yao kulingana na njia ya Shariah ya Kiislamu na sio njia ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

Mfano mwengine wa uzembe kama huo ni wakati moja ya miji ya nchi za Kiislamu inapoingia chini ya shambulzi la kijeshi, watengenezaji wa maalumati ya vyombo vya habari, kwa ikhlasi yao, wanamshambulia mvamizi na kuonyesha mshikamano na yule anayeshambuliwa, lakini badala ya kuelekeza Ummah katika majibu ya kurudisha shambulizi la kafiri kupitia kuhamasisha majeshi ya Waislamu, badala ya marekebisho haya, wanaizingira rai jumla katika Umma wa Kiislamu kwa kampeni ambazo zinaifedhehi rai jumla huko Magharibi, halafu wanatoa wito kwa nchi za ulimwengu, haswa za makafiri na nchi za wakoloni za Magharibi, kuingilia kati kusitisha vita! Wakati lilikuwa jukumu lao kuhamasisha rai jumla katika Ummah kutambua kwamba ulinzi wa miji ya Waislamu unapaswa kufanywa na majeshi ya Waislamu yaliyowekwa katika kambi zao.

**Enyi Waundaji Rai Jumla katika Umma wa Kiislamu:**

Sisi katika Hizb ut Tahrir tunakumbusheni wajibu mlio nao kwa Umma wa Kiislamu kwa kuusaidia kwa kuupatia fikra safi ya Kiislamu. Hizb ut Tahrir inaweka mikononi mwenu maalumati ya kifikra ya kisiasa, yaliyovuliwa kwa njia ya nguvu ya dalili kutoka kwa machimbuko ya sheria ya Kiislamu. Ndani yake, yanawasilisha maoni ya Shariah kuhusu changamoto za kifikra na kisiasa na yanawasilisha masuluhisho ya Shariah kwa maswala ya kisasa yanayoukabili Ummah. Kwa hivyo kuweni waangalifu, Enyi wamiliki wa majukwaa na waundaji wa rai jumla, kuweni waangalifu msiupatie Umma uzoefu wa kisiasa ambao roho zinautamani, ambao utazipotosha nafsi mkapotea na watu wakapotea pamoja nanyi. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

لِيَحْمِلُوا أَوْزَارَهُمْ كَامِلَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَمِنْ أَوْزَارِ الَّذِينَ يُضِلُّونَهُم بِغَيْرِ عِلْمٍ أَلَا سَاءَ مَا يَزِرُونَ

“Ili wabebe mizigo yao kwa ukamilifu Siku ya Kiyama, na sehemu ya mizigo ya wale wanao wapoteza bila ya kujua. Angalia, ni maovu mno hayo wanayo yabeba!” [An-Nahl: 25].

**Allahu Akbar Allahu Akbar Allahu Akbar La Ilaha Ila Allah… Allahu Akbar Allahu Akbar Wa Lilahi Alhamd**

Eid Mubarak, Wassalam Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

**Mh. Salah Eddine Adada**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



Email: info@uqab.or.ke

# Ukatili wa Kijinsia ni Natija ya Sera ya Usawa wa Kijinsia ya Kimagharibi

Mnamo Jumatano, 30 Juni 2021, Rais Uhuru Kenyatta alikemea kukithiri kwa idadi kubwa ya ukatili wa kijinsia barani Afrika, kwa kusema kuwa viwango vimefikia vya dharura duniani. Alizungumza hivyo katika majadiliano ya jopo katika ufunguzi wa kikao cha Kongamano la Kizazi Sawa (GEF) huko Paris, Ufaransa. GEF ni mjumuiko wa kimataifa wa usawa wa kijinsia ulioitishwa na Wanawake wa Umoja wa Mataifa na mwenyeji wake wakiwa ni Mexico na Ufaransa. Suluhisho alisema ni kuweka sera na kanuni madhubuti zenye kupambana na janga hili pamoja na kuzidisha ufadhili katika kulitatua. (The Standard, 30/06/2021)

Rais alisema kwamba Cameroon ina asilimia 35, South Afrika asilimia 37, Jamhuri ya Afrika ya Kati asilimia 50, Liberia asilimia 50 na Kenya asilimia 50 za viwango vya ukatili wa kijinsia na kwamba zimerekodi idadi kubwa hususan katika miezi kumi na mbili iliyopita ndani ya hichi kipindi cha Covid-19. Itakuwa ni ukosefu wa akili kujadili natija au matunda ya mti pasina kuwekeza umakini kwa mizizi yake. Kwa maana nyingine ni muhimu kufahamu chanzo cha janga la hili la ukatili wa kijinsia na kujua ni njia ipi sahihi ya kutatua tatizo hili. Hivyo basi, ni vyema kudadisi historia ya mwito wa kijinsia ili tujue mwanzo wake na mpaka ilipofikia hivi sasa.



Christine de Pizan alizaliwa kama mtoto wa pekee 1364 M mjini Bologna, Italia na kukulia, kuishi na kufariki 1430 M mjini Paris, Ufaransa. Babake, Tommaso di Benvenuto da Pizzano aliyejulikana kama Thomas de Pizan alikuwa ni daktari, mtu wa kutabiri siku zijazo na mshauri katika baraza la Venice huko Italia. Babake aliteuliwa kuwa mtabiri wa ziku zijazo wa mfalme Charles wa Tano wa Ufaransa na kuhamia Paris, Ufaransa. Mwaka 1368 M Christine alihamia Ufaransa na mwaka 1379 M akiwa na miaka 15 aliolewa na mthibitishaji na katibu wa ufalme Etienne du Castel.

Mwaka 1389 M mumewe Christine alifariki na mwaka kabla yake babake alikuwa amefariki. Kwa hiyo, Christine alilazimika kuwasimamia mamake pamoja na watoto wake watatu aliokuwa amewazaa. Aliisimamia familia yake kwa mali chache aliyoiwacha mumewe na kupitia malipo ya uandishi wake. Mwaka 1405 M aliandika kitabu kwa jina **Kitabu cha Mji wa Wanawake** kikiwa ni jibu kwa kitabu kilichoandikwa na kiongozi wa kanisa na mtunzi wa mashairi Mathieu wa Bologna kikiitwa **Maombolezo ya Matheolus**. Mathieu kupitia kitabu chake alidai kuwa ndoa / 'wanawake' wanawafanya wanaume kuishi maisha duni. Christine kupitia kitabu chake aliwatetea wanawake kwa kudai kuwa ndoa baina ya mwanamume na mwanamke ni ushirika wa usawa, na kuwataja wanawake kadhaa kama mfano wa kuigwa.

Pia aliongezea kuwa wanawake wamekuwa nyuma katika kila nyanja ya maisha kutokana na mpangilio wa mujtama unaompa kipaumbele mwanamume na kumtelekeza mwanawamke.

Christine de Pizan alikuwa ni katika watu wa tabaka la juu katika mujtama zama zake. Baada ya kuchapishwa kitabu chake hicho na vinginevyo ndipo alipoanza kuingia katika mvutano na viongozi wa makanisa karne hizo. Viongozi wa makanisa walimpinga kwa kuwa walibeba imani kwamba lengo la ndoa ni kuendeleza kizazi na kwamba mujtama wao uliokuwa umetawaliwa na wanaume na kuwataka wanawake kujisalimisha. Tokea zama hizo Christine de Pizan amekuwa akirudiwa na kuwa kiigizo cha wanaharakati na kila anayedai kutetea haki sawa za wanawake katika zama hizi ambapo mwito wa usawa wa kijinsia umeshamiri duniani kote.

Usawa wa kijinsia unaopigiwa debe na wa Magharibi hivi sasa duniani kote na ambao eti unalenga kuwakomboa wanawake katika utumwa wa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kielimu. Ukombozi huo unaolenga kuwapa wanawake uhuru usiokuwa na mipaka ili kufikia malengo yao kwa mujibu wa akili zao zinavyowatuma. Muasisi wa ukombozi wa wanawake leo karne ya ishirini ni Muamerika Betty Friedan, anayatambulika kwa kitabu

***Endelea... UK 6***

chake kiitwacho **Siri ya Uke**. Kupitia kitabu chake anadai kwamba lau wanawake wa nyumbani wa Amerika watachangamkia taaluma za kudumu, watakuwa na furaha na afya zaidi, ndoa bora na watoto wao watastawi.

Madai yake hayo ni kinyume na hali halisi ilivyo kwa kuzingatia takwimu zenye kutamausha na zinazoendelea kuzidi. Takwimu zinafichua mporomoko wa maadili, kuvunjika kwa familia, kuzidi kwa uzinifu na maovu mengi yote yakisababishwa na miito ya ‘usawa wa kijinsia’ ulimwenguni. Wanadamu wamevuka mipaka na kuwa kama wanyama! Hakuna haya wala stara kwani kila mmoja anakwenda mbio kufikia usawa wa kijinsia. Kiasi kwamba wanawake wanatembea uchi wakidai miili yao chaguo lao!

Tukitoa mifano baadhi ya matukio nchini Kenya, tafiti za miaka ya karibuni zinaonesha vurugu za ndani ya majumba zinaendelea kuzidi kila uchao. (The Star, 06/04/2021) Katika Kaunti ya Kirinyaga mnamo Jumatatu, 28 Juni 2021 makasisi kutoka katika kanisa la Anglican waliweka wazi kwamba kuna ongezeko la visa vya mizozo ndani ya majumba huku wanaume wakidaiwa kupigwa na kufurushwa na wake zao. (k24tv.co.ke, 28/06/2021) Kwa kuongezea huko Kaunti ya Embu, wanaume ndani walioowa walipaza sauti zao kuwa wanadhulumiwa kimwili na kukosa haki zao za ndoa. Samuel Muturi ambaye ni mwenyekiti wa kikundi cha Inua Wazee alisema kwamba ‘Tunakabiliwa na wakati mgumu ndani ya familia zetu; hatufurahii ndoa. Tunaiomba serikali kuwawezesha wanaume na kuweka mpango sawa katika kuamiliana wanaume na wanawake ndani ya kaunti.” (The Star, 03/06/2021) Ama tukivuka na kwenda nchi jirani na ng’ambo hususan katika mataifa yanayodai kuwa zimeendelea katika kuwapa raia wake uhuru kama Amerika, Ufaransa, Uingereza, Ujerumani n.k. Mashaka na vilio vimeshamiri pasina kupatikana suluhisho msingi!

Hali hizo za mashaka na vilio zitaendelea kuwa hivyo kwa sababu wanadamu wamejitenga na muongozo wa Muumba wao (swt). مَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِى فَإِنَّ لَهُۥ مَعِيشَةً ضَنكًا وَنَحْشُرُهُۥ يَوْمَ ٱلْقِيَـٰمَةِ أَعْمَىٰ “Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.” [Ta Ha:124]. Katika mchakakato wa kupigia debe usawa wa kijinsia wa Magharibi pamoja na watawala vibaraka ulimwenguni wamefaulu kumakinisha fikra za mujtama huria. Wahanga wakubwa wakiwa ni Waislamu walioweza kuupiga vita Uislamu kwa kuitukuza itikadi ya kisekula yenye kutenganisha dini na maisha. Wakiona kwamba kufanya hivyo ndio kuendelea, kufaulu na kuwapatia umaarufu. Kinyume chake ni kuzama ndani ya makaa ya moto wa kihuria!

Leo imefikia kiasi cha wazee kwa vijana Waislamu kutekwa nyara kifikra na wa Magharibi kwa sura eti ya kuwakomboa kwa kuwapa elimu ya kisekula. Kisha hatimaye kuwapa tuzo za kimatiafa na dori ya kuwa mabalozi wa usawa wa kijinsia na elimu ya kisekula ulimwenguni. Ili kufikia malengo yao hutoa kauli hadaifu zenye kupiga vita taasisi ya ndoa. Kwani ndoa ni moja katika mawe msingi katika ujenzi wa mujtama na kizazi kwa ujumla. Lengo likiwa ni kuhakikisha watu wanabakia kuwa kama wanyama wanaoshiriki ufuska kwa shinikizo la usawa wa kijinsia na kufurahia uhuru wao.

Mfano ni kauli ya hivi majuzi ya mwanaharakati na mshindi wa tuzo ya Amani ya Nobel, Malala Yousafzai alisema, **“Bado mimi sielewi kwa nini watu wanapaswa kuoana. Ikiwa unataka kuwa na mtu katika maisha yako, kwani yapasa muweke saini karatasi za ndoa, kwa nini isiwe tu ni ushirika?”** Hayo yakiwa ni sehemu ya matamshi yake katika mahojiano na Jarida la Vogue Toleo la Julai 2021. (www.vogue.co.uk, 01/06/2021) Na kupitia matamshi kama hayo kutoka kwa wanaodaiwa ni watetezi wa ukombozi wa wanawake ambao wameandaliwa na kuwekewa mazingira ikiwemo pamoja na kupewa fursa na vyombo vya habari vya wa Magharibi ili kuendeleza fikra za mujtama huria.

Hakika vurugu za kijinsia hazikuwahi kushuhudiwa chini ya utawala wa Dola ya Kiislamu. Kwani Uislamu ukiwa ni mfumo kamili wa maisha unaotoka kwa Muumba wa ulimwengu, mwanadamu na uhai. Umepangilia kwa makini majukumu na haki za mwandamu katika uhai wake. Vile vile Muumba akawaumba wanadamu kwa jinsia ya kike na kiume ili iwe ni rehema kwa wanadamu na wala sio kwa ajili ya kusababisha vurugu kama inavyoshuhudiwa leo chini ya mfumo batili wa kirasilimali. وَمِنْ ءَايَـٰتِهِۦٓ أَنْ خَلَقَ لَكُم مِّنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَٰجًا لِّتَسْكُنُوٓا۟ إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُم مَّوَدَّةً وَرَحْمَةً ۚ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَـَٔايَـٰتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ “Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri.” [30. Ar-Rum: 21] Kwa hiyo uumbaji wa jinsia ya kike na kiume sio kwa ajili ya kuleta ushindani na mizozo badala yake ni kuletea utulivu na amani katika mujtama kupitia mume na mke kuoana kwa mujibu wa Shari’ah ya Kiislamu.

Uislamu unawahesabu mwanamume na mwanamke kuwa wako sawa mbele ya Shari’ah. Zaidi ya hayo Uislamu ukawapa haki sawa mwanamume na mwanamke ikiwemo haki za kushiriki katika kumchagua mtawala, kumiliki mali, kuajiri, kuajiriwa, kufanya biashara n.k. Haki ambazo kiasili zimekuwepo kwa takribani zaidi ya karne 13 na zitabakia mpaka Siku ya Kiyama. Wakati wa Magharibi wamezama ndani ya kiza cha mporomoko wa kihadhara, mwanamke alikuwa ni mtumwa anayetumika kama chombo cha kujistarehesha asiyekuwa na haki ya kushiriki uchaguzi (kuchagua au kuchaguliwa), kumiliki mali, kuajiriwa, kuajiri n.k. Ilhali upande wa pili, wanawake katika Uislamu walikuwa wanashiriki kikamilifu katika siasa ya kiwango cha juu katika mfano ni kumpa mkono Mtume(saw) katika kiapo cha ahadi ya utiifu (Ba’yah al-Aqaba) kuwa mtawala wao. Miongoni mwa walioshiriki ni wanawake wawili ambao

***Endelea... UK 7***

 Email: info@uqab.or.ke

ni Umm Umara Nasiba na ambaye alikuwa akifanya kazi kama muuguzi na Umm Mani, Asma. Wanawake wengine wengi wamewapa Ba'yah makhalifah na kushiriki upiganaji 'Jihad' kuilinda Dola ya Kiislamu kwa karne nyingi mno.

Ama upande wa haki za kielimu, wanawake wengi akiwemo Umm al-Darda al-Kubra (ra). Alikuwa ni mwanachuoni bingwa katika Karne ya Saba huko Sham. Alifundisha katika sehemu ya wanaume msikitini na alikuwa mwalimu wa hadith na fiqh. Miongoni mwa wanafunzi wake alikuwa ni Khalifah Abd al-Malik ibn Marwan. Mwingine ni Hafsa bint Sirin (rh) miongoni mwa tabieen alikuwa mwanachuoni aliyeishi na kufunza huko Basra. Fatima bint Muhammad al-Fihriyya al-Qurashiya alikuwa ndiye muasisi wa Msikiti wa al-Qarawiyyin mnamo 859 M. Msikiti ambao baadaye ulikuwa ni taasisi ya masomo na inayotambulika kuwa chuo kikuu cha kwanza duniani.

Kiuchumi wanawake wameruhusiwa na Shari'ah kuajiriwa, kuajiri, kufunga mikataba, kuwakilisha/ kuwakilishwa katika mikataba ya kibiashara, kushiriki kilimo n.k. Lakini suala zima la uchumaji kwa ajili ya kuisimamia familia ni jukumu la babake, mumewe au msimamizi wake na sio mwanamke mwenyewe. Kufanyakazi kwa mwanamke sio lazima japo ameruhusiwa na Shari'ah (mubah). Mshahara au malipo yake ni yeye ndiye anayeamua atakavyotumia kwa mujibu wa kipimo cha halali na haramu na hashurutishwi kufanya kazi wala kutoa matumizi. Mwanamke ni tunu inayostahiki, kuheshimiwa, kulindwa na kuhifadhiwa kutokana jukumu muhimu alilopewa na Muumba. Mwenyezi Mungu (swt) amempa jukumu la kuwa mke na mama. Ambaye kazi zake ni ndani ya nyumba yake ni kazi za nje zikiwa za mumewe.

Kinyume chake leo mwanamke ametolewa ndani ya nyumba yake na kufanywa mtumwa wa hawa'a za nafsi yake. Kwa kujisalimisha kwa mchoro wa Magharibi wamiliki wa makampuni na viwanda vinavyokwenda mbio kupatiliza idadi kubwa ya wanawake duniani. Eti naye mwanamke amekuwa anapigana vikumbo na wanaume katika uchumaji tonge la familia. Huku akili yake na mawazo yake ni kumpiku mumewe katika uchumaji ili awe ndiye mwenye usemi na kuendesha mambo ndani ya familia! Watoto na majumba yakitelekezwa kupindukia. Katika mchakato huo wanawake wanapigiwa debe na kusifiwa na vyombo vya habari na kupongezwa eti ni wanawake wachapakazi shupavu na mfano wa kuigwa. Na wakati huo huo vikidunisha umama kuwa ni mzigo na kikwazo kwa mwanamke kutofurahia maisha na uhuru wake. Si hayo tu, kila kukicha kunazuka mapya, kiasi kwamba leo imefikia hata mwanamke kuamua siku ya kukutana na mumewe na kinyume chake mara mwanamke anamshitaki mumewe kwa kosa la kumbaka! Ilhali ni haramu kwa mke kutoitikia ombi la mumewe anapomuhitaji katika malazi!

Natija yake ni maangamivu ya kupindukia yanayoendelea hadi sasa na yanayoshuhudiwa na kila mmoja duniani. Kusita kwa hali hii ni pale ambapo wanadamu na hususan Waislamu duniani watakapozinduka na kuona kuwa usawa wa kijinsia ni fikra potofu na hatari kwa mujtama. Hatimaye washikamane na kujiunga na harakati yenye kufanyakazi ya kuregesha tena maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha Serikali ya Kiislamu ya Khilafah kwa njia ya Utume. Ni kupitia Khilafah ndipo mwanamke atakuwa ni tunu ya kweli yenye kustahili kuheshimiwa, kulindwa na kuhifadhi. Jukumu la umama litapewa cheo na kufanyiwakazi barabara ili kuandaa kizazi chenye utambulisho (shaksiyyah) madhubuti wa Kiislamu. Kizazi ambacho kitamtwii Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume wake (saw) na kuwaheshimu na kuwaenzi wazazi wao kwa kwa kujisalimisha kwa maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu (swt).

Khilafah pekee ndio yenye uwezo wa kukomesha kimsingi ukatili wa kijinsia kwa kuwafurusha wa Magharibi wakoloni kutoka katika ardhi za Waislamu na kuitupilia mbali hadhara yao iliyojikita katika itikadi ya kutenganisha dini na maisha / serikali. Khilafah itakwenda mbio kuwaandaa na kuwajenga mabinti shupavu wenye kuthamini haki na kuridhika na majukumu msingi waliowekewa na Mwenyezi Mungu (swt). Napia kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika nyanja za maisha ikiwemo kuwa wavumbuzi na wanachuoni mahiri. Na wala sio kuwafanya kuwa kizazi cha Z kama kinavyojulikana hivi sasa. Kizazi kinachotambulika kwa sifa ya kuogolea ndani ya bahari ya uhuru wa kupindukia!

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Tume ya Uajiri wa Walimu (TSC)

https://www.standardmedia.co.ke/education/article/2001414062/tsc-plans-to-hit-education-graduates-hard

Tovuti ya Standard (kiunga hapo juu) iliandika makala yenye kichwa "TSC ina mpango wa kuwakomoa kwa kishindo mahafali wa taaluma ya elimu"

“Kwa mujibu wa mapendekezo mapya yaliyotolewa na Tume ya Uajiri wa Walimu (TSC), mahafali wote wa chuo kikuu wanaokusudia kufundisha watalazimika kupata cheti cha diploma ya ualimu”

**Katika kuongeza na kuifanya vigumu zaidi nafasi ya kuingia katika taaluma ya ualimu (TC). Tutataja mambo 3 tu:**

1. Lazima cheti (Stashahada ya Elimu baada ya kuhitimu chuoni) kabla ya zoezi la kufundisha. “Wanafunzi wote wa 8-4-4 na Mtaala wa Umilisi (CBC) lazima wafanye kwanza, Shahada ya Sanaa au Shahada ya Sayansi kwa kipindi cha miaka mitatu inayoangazia masomo muhimu na, baada ya hapo, kufanya Stashahada ya Ualimu kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa ajili ya kufundisha katika shule ya Upili ya daraja la chini na la juu na SNE (Elimu ya Mahitaji Maalum), ” hati hiyo inasema.” (Kiunga hapo juu)

2. Kuongeza kiwango cha elimu kutoka cheti hadi stashahada katika taaluma ya Ualimu kabla ya kuajiriwa. "Mapendekezo mengine ni kwamba kiwango cha chini cha kuingia katika taaluma ya ualimu nchini Kenya katika ngazi zote kitakuwa stashahada katika Ualimu."

3. Kutokana na nakisi ya kifedha baada ya covid, wanataka kupunguza idadi ya wanafunzi wanaodhaminiwa na serikali kwa kuiita "ziinaongozwa na mahitaji". "Wakati huo huo, usajili katika diploma zote na digrii zote katika kozi za ualimu zitakuwa" zinaongozwa na mahitaji ", ikimaanisha kwamba idadi ya waalimu wanaohitimu kila mwaka itadhibitiwa." (Kiunga hapo juu)

**Sababu za mabadiliko haya makubwa, Mkurugenzi wa Uhakiki wa Ubora na Viwango katika TSC, Dk Reuben Nthamburi alidokeza kuwa:**

1. "Kwamba kuna stashahada ya diploma katika elimu ya upili ambayo itashughulikia sehemu maalumu za kusomwa / masomo yanayotakiwa katika daraja la chini na la juu la upili ambayo yana upungufu." (Kiunga hapo juu)

**Upinzani:**

1. Jana, Chama cha Wafanyakazi wa Vyuo Vikuu (UASU) kilielezea kutoridhishwa na yaliyomo kwenye waraka huo.
"Wanataka kuondoa programu ya Digrii ya Elimu ili wanafunzi wote wajisajili tu kwa Shahada ya Sanaa au ya Sayansi. Wanapohitimu na mmoja akapendelea ualimu, lazima arudi kupata diploma ya ualimu,”akasema Dkt Wilfridah Itolondo, makamu mwenyekiti wa UASU wa Chuo Kikuu cha Kenyatta.

2. “Wahadhiri wa vyuo vikuu wanahisi huu unaweza kuwa mpango wa kutekeleza kiujanja mapendekezo ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kuhusu kupunguza bajeti na matumizi katika baadhi ya mashirika ya serikali, ambayo yanaweza kuhusisha kusitisha uajiri mpya au kushinikiza kupunguzwa kwa wafanyakazi kama kigezo kwa Kenya kupewa mkopo wa bilioni Sh 257”(Kiunga hapo juu)

**Athari za utekelezaji wa pendekezo la TSC utasababisha yafuatayo:**



Email: info@uqab.or.ke

1. Kupunguza fedha kwa sekta ya elimu

2. Kusambaratisha zaidi huduma katika shule za umma ambazo zinategemewa na wananchi wengi.

3. Baada ya vizuizi vya Covid, Wakenya wengi wamehamia katika shule za Umma kupunguza matumizi ya lazima. Kwa hivyo, kuongeza haja "inayoongozwa na mahitaji" badala yake nafasi zaidi hutolewa kwa kozi za kufundisha.

4. Kulazimisha watu kwenda shule za kibinafsi kwa sababu ya nafasi ambazo hazipatikani katika shule za umma. Au kurundika kwa wanaufunzi katika shule za umma kusiko na ufanisi wa kielimu ambako kutaongeza tu wasiojua kusoma na kuandika na raia wasio na ujuzi wowote. Mzigo kwa Wakenya wengi utazidi kuongezeka wakimezea mate utajiri unaokusanywa na wasomi.

**Hizi ni athari zinazoendelea za ubepari ulimwenguni. Uislamu na mfumo wa Khilafah una uwezo na rahma ya kuwainua raia wake kwa utulivu na faraja.**

1. Udhibitisho au idhini (Ijazah) katika Uislamu inahusishwa na mwalimu sio taasisi ambayo inaweza kudanganya kwani inategemea wafanyikazi, uwezo wa kifedha na mengine, ambayo hutofautiana mara kwa mara. Hii inafanya msururu wa walimu ujulikane ambao husaidia kufafanua ukweli na kudumisha usafi wa yaliyomo.

2. Kwa ubepari, serikali haiwajibiki kuhakikisha mahitaji ya msingi ya kila mtu yametimizwa. Inachanganya mahitaji (pamoja na elimu ambayo ni somo) na mahitaji ya ziada (tunayoweza kuishi bila) kwa hivyo huona (mahitaji msingi na mahitaji ya ziada) kama ambayo hayatoshelezeki kwa kila mtu.

3. Ufadhili wa SGR na miradi mingine kabambe ipo hata mikopo inachukuliwa kuiwezesha kutekelezeka na katika sekta ya elimu tunashuhudia kupunguzwa kwa bajeti. Hivi ndivyo ambavyo ubepari unalipa kipaumbele suala la uzalishaji juu ya usambazaji kwa sababu miradi ya miundombinu huongeza uzalishaji na kupunguza mzigo wa vifaa. Uislamu unatanguliza usambazaji juu ya uzalishaji. Kwa hivyo, ukaruhusu hata ushuru kwa utajiri wa matajiri (ikiwa hazina ya serikali haitoshi) kwa kukidhi mahitaji ya kimsingi ya raia wake.

4. Mikopo yenye riba kila wakati imekuwa mzigo kwa watu wa chini katika jamii tangu enzi za utumwa. Sio mengi yamebadilika hivi leo, mikopo ni moja ya minyororo inayotumiwa kuzifunga nchi za "ulimwengu wa tatu" kujinasua kutoka kwa ukoloni.

5. Uislamu umetungwa sheria na Mwenyezi Mungu (SWT) ambaye haitaji rasilimali ili kuishi. Tofauti na kibepari ambayo inatuacha tukigombania mabaki ya mkoloni, watawala wasomi na wandugu.

6. Uislamu umewekewa sheria na Mwenyezi Mungu (SWT) ambaye hahitaji rasilimali ili kuishi. Tofauti na mabepari ambao wanatuacha tukigombania mabaki ya mkoloni, watawala na marafiki zao.

**Na Samira Mohamad Ali**

MSOTO WA KIUCHUMI

UISLAMU NDIO JIBU

*Kuweni pamoja na wafanyakazi wa kusimamisha Khilafah Rashidah kwa njia ya Utume.*

HIZB UT-TAHRIR KENYA

Sheria juu ya uchumi katika Uislamu zimejengwa juu ya nguzo tatu:-

- Asili ya umiliki
- Umilikishwaji
- Mzunguko wa mali baina ya watu

**#Msoto_wa_kiuchumi_Uislamu_ndio_jibu** 18

MSOTO WA KIUCHUMI

UISLAMU NDIO JIBU

*Kuweni pamoja na wafanyakazi wa kusimamisha Khilafah Rashidah kwa njia ya Utume.*

HIZB UT-TAHRIR KENYA

Uislamu umefanya azma ya kumiliki mali kuwa njia ya kutosheleza mahitaji na si kwa malengo ya majivuno. Pia umefanya usimamizi wa uchumi kwa ujumla kuendeshwa kwa amri za Allah kuwa jambo la lazima.

**#Msoto_wa_kiuchumi_Uislamu_ndio_jibu** 17



Email: info@uqab.or.ke

MSOTO WA KIUCHUMI
UISLAMU NDIO JIBU

*Kuweni pamoja na wafanyakazi wa kusimamisha Khilafah Rashidah kwa njia ya Utume.*

HIZB UT-TAHRIR KENYA

Mfumuko wa bei ni tatizo la mara kwa mara ndani ya mfumo wa kibepari, uliochukua mfumo wa pesa za makaratasi zisizokuwa na faida halisi, kwani haiwezi kubadilishwa kwa kitu chochote chenye kushika. Tatizo hili ni silaha zinazotumiwa kudhibiti usambazwaji wa bidhaa na huduma katika mfumo wa kirasilimali.

**#Msoto_wa_kiuchumi_Uislamu_ndio_jibu** 9

MSOTO WA KIUCHUMI
UISLAMU NDIO JIBU

*Kuweni pamoja na wafanyakazi wa kusimamisha Khilafah Rashidah kwa njia ya Utume.*

HIZB UT-TAHRIR KENYA

Usekula (Kutenganisha dini na maisha, siasa na serikali) ndio msingi uliojengwa juu yake nidhamu zote za kimaisha za mfumo wa kirasilimali, ikiwemo nidhamu yake ya kiuchumi na msingi huo ndio chanzo halisi cha kuenea msoto wa kiuchumi kote ulimwenguni.

**#Msoto_wa_kiuchumi_Uislamu_ndio_jibu** 8


Email: info@uqab.or.ke

MSOTO WA KIUCHUMI

UISLAMU NDIO JIBU

*Kuweni pamoja na wafanyakazi wa kusimamisha Khilafah Rashidah kwa njia ya Utume.*

HIZB UT-TAHRIR KENYA

*Uzalishaji wa uchumi katika serikali za Kirasilimali ni dhana hadaifu isiyo na mashiko kwa sababu huakisi (hauoneshi) hali halisi ilioko mashinani. Utasikia kwa mfano uchumi wa Kenya umekua kwa asilimia 10 na ilhali nchi yenyewe inadaiwa malimbikizi ya madeni ya nje na ndani huku mafukara na masikini wakizidi kuongezeka kwa kiwango cha kutisha kila uchao!*

**#Msoto_wa_kiuchumi_Uislamu_ndio_jibu** 2

MSOTO WA KIUCHUMI

UISLAMU NDIO JIBU

*Kuweni pamoja na wafanyakazi wa kusimamisha Khilafah Rashidah kwa njia ya Utume.*

HIZB UT-TAHRIR KENYA

*Katika mfumo wa Kirasilimali suala la ubinafsishaji wa nyenzo za uzalishaji hupokonya wanadamu njia msingi ya kumpa ufanisi na utambulisho imara wa Kiuchumi. Kwa mantiki hii ndio hujikuta mfanyikazi kwamba kazi yake ni njia ya kukabiliana na maisha huku asiambulie chochote kazini, hii ni kwa sababu faida/tija ya kazi yake sio yake yeye bali ni ya mwajiri wake.*

**#Msoto_wa_kiuchumi_Uislamu_ndio_jibu** 3